Kanuni na Masharti ya Kutumia BizFundi

Mara ya mwisho kupitiwa: 17 Mei, 2018

Tafadhali soma Kanuni hizi za Matumizi ("Kanuni", Kanuni za Matumizi") kwa uangalifu kabla ya kutumia tovuti ya www.bizfundi.or.tz na programu ya simu ya Bizfundi (kwa pamoja au kila kimoja peke yake, inayotajwa kama "Huduma") inayoendeshwa na International Executive Service Corps ("nasi", "sisi" au "yetu").

Kanuni na Masharti haya yanahusu tovuti na sehemu zake zote, matawi, na tovuti za mitandao yote shiriki inayofanya rejea kwayo.

Upataji na matumizi yako ya Huduma vina sharti la wewe kukubaliana nazo na kuheshimu kanuni hizi. Kanuni zinawahusu wote wanaotembelea, watumiaji, na washiriki wengine wenye nia ya kupata au kutumia Huduma hii.

Kwa kuingia kwenye Tovuti, unathibitisha kuwa unazielewa Kanuni na Masharti yake. Kama haukubaliani na Kanuni na Masharti haya ya matumizi unaweza kutoumia tovuti hii. Tovuti ndiyo yenye haki ya kubadili, kuboresha, kuongeza, au kuondoa sehemu za Kanuni na Masharti ya matumizi wakati wowote ule. Mabadiliko yataanza kutumika mara yatakapotumwa kwenye Tovuti bila ya kutolewa taarifa yoyote ile. Tafadhali, pitia Kanuni na Mashrati ya matumizi mara kwa mara ili kubaini kama kuna jambo lolote jipya. Kuendelea kutumia Tovuti hata baada ya kutumwa kwa mabadiliko kunadhihirisha ijapo sio kwa dhahiri kukubaliana kwako na mabadiliko husika

Mawasiliano

Kwa kuwa na Akaunti kwenye huduma yetu, unakubali kuagiza majarida, makala za kutangaza au kukuza bisahara na taarifa nyingine yoyote tunayoweza kuituma. Hata hivyo, una hiyari ya kuomba kutopokea aina yoyote au aina zote za mawasiliano ya namna hii kutoka kwetu kwa kuwasiliana nasi kwa barua pepe bizfundi@iesc.org ikiwa na neno kwenye mstari wa mada, 'kujitoa'.

Maudhui ya Tovuti na Matumizi

Huduma yetu inakuruhusu kutuma, kujiunga, kuhifadhi, kutoa kwa mwngine na vinginevyo kufanya taarifa fulani, maandishi, michoro, video, au makala zingine ('Maudhui") iweze kupatikana. Unawajibika kwa Maudhui unayotuma kwenye Huduma hii au kupitia kwayo, ikiwemo uhalali wake kisheria, uaminikaji, na usahihi wake.

Ukiukaji wowote wa Kanuni na Masharti utapelekea kufutwa mara moja kwa leseni iliyotolewa kwenye ibara hii bila ya wewe kupewa taarifa yoyote. Maudhui yatolewayo kwenye tovuti hii ni kwa lengo la kuhabarisha peke yake. Mawasilisho au maoni yatolewayo kwenye Tovuti hii ni ya washiriki binafisi wanaotuma maudhui hayo na wala hayawakilishi maoni yetu. Baadhi ya Huduma fulani na vipengele vinavyoendena navyo vinavyoweza kupatikana kwenye Tovuti vinaweza kuhitaji kujiandikisha au kujiunga navyo. Ikiwa utachagua kujiandikisha au kujiunga kwenye huduma yoyote ya aina hiyo au vipengele vinavyohusiana navyo, basi utakuwa unakubali kutoa taarifa sahihi na ya hivi karibuni kuhusu wewe binafsi, na kukubali kuifanyia mabadiliko haraka taarifa hiyo mara pale mabadiliko yanapotokea kwenye taarifa hiyo.

Kila mtumiaji wa Tovuti anawajibika yeye binafsi kutunza maneno siri na Vitambulisho vingine vya ulinzi na usalama wa akaunti. Mwenye Akaunti anawajibika kikamilifu kwa shughuli zote zitakazofanyika kwenye nenosiri au akaunti hiyo. Vilevile, unapaswa kutuarifu pale unapobaini kuwapo kwa matumizi yasiyoidhinishwa ya nenosiri au akaunti yako. Tovuti haitawajibika au kuwa na dhima, moja kwa moja au vinginevyo, kwa namna yoyote ile kwa hasara au uharibifu wa aina yoyote uliosababishwa na au kuhusiana na kushindwa kwako kuzingatia kipengele hiki. Wakati wa mchakato wa kujiandikisha unakubali kupokea barua pepe za matangazo ya biashara kutoka kwenye tovuti hii. Unaweza hatimaye kujitoa kwenye upokeaji wa barua pepe za matangazo ya biashara kwa kubofya kwenye anwani ya matandao iliyo chini ya kila barua pepe ya tangazo la biashara.

Kwa kutuma Maudhui kwenye au kupitia Huduma hii, unaonesha na kuthibitisha kuwa: (i) Maudhui ni yako (unamiliki) na/au una haki ya kuyatumia na haki ya kutupa sisi haki na leseni kama kwenye Kanuni hizi, na (ii) kwamba utumaji wa Maudhui yako kwenye au kupitia Huduma hii hakukiuki haki ya faragha ya mtu, haki za utangazaji, haki miliki, haki ya mkataba au haki nyingine zozote za mtu au taasisi yoyote. Tunabaki na haki ya kusimamisha akaunti ya mtu yeyote atakayeonekana kukiuka haki miliki

Unabaki na haki yoyote na haki zote za Maudhui yoyote unayowasilisha, kutuma au kuonesha kwenye au kupitia Huduma na unawajibika katika kuzilinda haki hizo. Hatuchukui jukuma na kubeba dhima kwa Maudhui ambayo wewe au mshiriki mwingine yeyote anatuma kwenye au kupitia Huduma hii. Hata hivyo, kwa kutuma

Mauhdui kupitia Huduma hii unatupa haki na leseni ya kutumia, kuboresha, kuitekeleza kwa umma, kuionesha kwa umma, kudurufua, na kusambaza maudhui hayo kwenye na kupitia Huduma hii. Unakubali kuwa leseni hii inahusisha haki ya sisi kuyafanya Maudhui yako yapatikane kwa watumiaji wengine wa Huduma, ambao wanaweza pia kutumia Maudhui yako kwa kufuata Kanuni hizi.

Kwa maaana hii basi, kila utakachowasilisha kwenye Tovuti au kututumia, ikiwemo ila haishii tu, kwenye maswali, tathmini, maoni na mapendekezo, (kwa pamoja 'Mawasilisho") vitakuwa mali yetu pekee na havitarudishwa kwako. Pamoja na haki inayohusu Wasilisho lolote, unapotuma maoni au tathmini kwenye Tovuti, pia unatupa haki ya kutumia jina unalowasilisha, linalohusiana na tathnmini, maoni au maudhui mengine. Hupashwi kutumia anwani ya barua pepe ya uongo, kujifanya ni mtu mwingine tofauti na wewe mwenyewe au vinginevyo kutupotosha sisi au washiriki wengine kuhusiana na chanzo cha Mawasilisho yoyote, vinginevyo utakabaliana na matatizo ya kisheria. Tunaweza, bali hatutalazimika, kuondoa au kuhariri Mawasilisho yoyote.

International Executive Service Corps ina haki bali sio wajibu wa kufuatilia na kuhariri Maudhui yote yanayoletwa na watumiaji.

Pamoja na hili, Maudhui yatakayokutwa kwenye au kupitia Huduma hii ni mali ya International Executive Service Corps au yatatumiwa kwa ruhusa. Hauto paswa kusambaza, kurekebisha, kutuma, kurudia matumizi, kupakua, kurudia kutuma, kunakili, au kutumia Maudhui husika, iwe yote kwa ujumla au sehemu yake, kwa malengo ya kibiashara au kwa manufaa binafsi, bila kwanza na dhahiri kuwa na ruhusa kimaandishi kutoka kwetu.

Upatikanaji wa Tovuti

Lengo letu ni kuhakikisha kuwa Tovuti yetu inapatikana wakati wote, hata hivyo, hatuthibitishi kwa namna yoyote kuwepo kwa jambo hilo na tunabaki na haki ya kusitisha Tovuti wakati wowote na bila taarifa. Kwa kukubaliana na Kanuni na Masharti yaliyowekwa, Unakubali kuwa huduma inaweza kukatishwa ili kuruhusu maboresho kwenye Tovuti, ukarabati wa kiratiba au kwa sababu nyingine zilizo nje ya uwezo wetu.

Matumizi Yanayoruhusiwa na Yanayokatazwa

Unaweza kutumia Huduma kwa lengo tu la kupashana na kubadilishana mawazo na Watumiaji wengine. Hautoweza kutumia Huduma kukiuka sheria zozote zilizopo za mahali ulipo, za nchi, za taifa, za kimaaifa, ikiwemo bila kujifunga kwenye sheria zozote zinazohusiana na kukosa imani au biashara zingine au mienendo ya kibiashara isiyo halali, sheria za kiusalama za shirikisho na za nchi, kanuni za

kisheria zilizotangazwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sheria zozote za kitaifa au mabadilishano yoyote ya kiusalama, na sheria na kanuni zote za kisheria zinazosimamia utoaji nje au uingizaji wa bidhaa au taarifa ya kiufundi.

Unaweza kutopaswa kupakua au kutuma makala yoyote inayokiuka au kuhodhi isivyo halali haki miliki ya mtu yoyote, haki ya miliki ya ugunduzi, nembo ya biashara au siri ya biashara, au kufichua kupita Huduma taarifa yoyote, ufichuaji ambao unaweza kupelekea ukiukaji wa majukumu ya utunzaji siri unayoweza kuwa nayo.

Unaweza kutopaswa kupakua virusi vyovyote, minyoo, farasi wa Trojan au mifumo mingine yenye madhara ya msimbo wa kompyuta, na wala kuuweka mtandano wa Tovuti au seva zake kwenye msongamano usiostahili wa taarifa, au vinginevyo kujiingiza kwenye mienendo inayochukuliwa kuwa ni uharibifu katika utendaji wa kawaida wa Tovuti.

Hauruhisiwi kabisa kufanya mawasiliano yoyote kwenye au kupitia Huduma hii, ya makala inayokiuka sheria, yenye kudhuru, kuchukiza, vitisho, lugha chafu, kukashifu, usumbufu, udhalilishaji, isiyo na maadili, matusi, kufuru, chuki, uongo, inayoashiria vitendo vya ngono, ubaguzi wa rangi, ukabila, au vinginevyo makala ya aina yoyote isiyokubalika, ikiwemo ingawa haishii tu kwenye makala inayohamasisha mienendo inayoweza kuwa ni kosa la jinai, inayoweza kusababisha dhima ya kijamii, au vinginevyo inayokiuka sheria yoyote iliyopo ya mahali husika, nchi, taifa, au kimataifa.

Pia hauruhusiwi kabisa kusambaza taarifa binafsi za Watumiaji kwa washiriki wengine kwa malengo ya kujinufaisha kibiashara. Tutachukulia ukusanyaji wa orodha ya matangazo ya biashara pamoja na anwani za wapokeaji kwa kutumia taarifa binafsi za Watumiaji, utumaji wa makala za matangazo ya biashara ambayo hayajaombwa kwa Watumiaji, au usambazaji wa taarifa binafsi za Watumiaji kwa washiriki wengine kwa malengo ya kutangaza biashara kuwa ni ukiukaji mkubwa wa Kanuni na Masharti ya Matumizi, na tunabaki na haki ya kusitisha au kusimamisha upatikani au matumizi ya Tovuti kwako na kusimamisha au kukuvua uanachama kwenye ushirika bila fidia ya ada zozote za uanachama zilizolipwa.

Tunatambua kuwa matumizi yasiyoidhinishwa ya taarifa binafsi ya Watumiaji, yanayohusiana na utumaji wa matangazo ya biashara ambayo hayajaombwa na mtumiaji, yanaweza pia kuchukuliwa kama ukiukaji wa amri na maagizo mbalimbali ya nchi na Jamhuri kuhusu mapambano dhidi ya spam. Tunabaki na haki ya kutoa taarifa ya matumizi mabaya ya taarifa ya Mtumiaji binafsi kwenye vyombo husika

vinavyosimamia sheria au mamlaka za serikali, na tutatoa ushirikiano wetu kikamilifu kwa mamlaka yoyote itakayochunguza ukiukaji wa sheria hizi.

Ukiukaji wa Mtumiaji

Tafadhali toa taarifa kwetu kuhusu matatizo yoyote yanayojirudia, maudhui ya kuchukizaku na ukiukaji wa sera. Tuanajitahidi kuhakikisha kuwa maudhui yote yanayotumwa hayakiuki haki miliki, nembo ya biashara au haki Miliki zingine zozote za washiriki wengine Ikiwa unaamini kuwa Haki Miliki zako zimekiukwa, tafadhali iarifu timu yetu na tunakuhakikishia kuwa tutaifanyia uchunguzi.

Akaunti

Unapofungua akunti na sisi, unathibitisha kuwa una umri usio chini ya miaka 18 au unaingia kwenye Tovuti chini ya usimamizi wa mzazi au mlezi anayetambulika kisheria na kwamba taarifa unayotupatia wakati wote ni sahihi, kamili, na ni ya hivi karibuni. Taarifa isiyo sahihi, isiyo kamili na iliyopitwa na wakati inaweza kupelekea kusitishwa mara moja kwa akaunti yako kwenye Huduma.

Tunakupatia leseni ambayo haitatumiwa na mtu mwingine, inayoweza kufutwa, na ambayo hautakuwa mshiriki pekee wa kutumia Tovuti, kulingana na Kanuni na Mashart yaliyoelezwa hapa, kwa lengo la kutafuta bidhaa zinazouzwa kwenye Tovuti. Matumizi ya kibiashara au matumizi kwa niaba ya mshiriki mwingine hayaruhusiwi, isipokuwa tu pale ruhusa itakapokuwa imeshatolewa na sisi mapema kabla yake.

Una wajibu wa kutunza siri ya akaunti yako na nenosiri lako, ikiwemo ila haishii tu kwenye kuzuia uingiaji kwenye kompyuta na/au akaunti yako. Unakubali kuwajibika kwa shughuli yoyote au zote au vitendo vitakavyotokea kwenye akaunti na/au nenosiri lako, bila kujali kama neno siri lako liko kwenye Huduma yetu au huduma ya mshiriki mwingine. Unapaswa kutupa taarifa mara tu utakapobaini kuwa kuna ukiukaji wa usalama au kuna matumizi yasiyoidhinishwa ya akaunti yako.

Hautoweza kutumia, kama jina la mtumiaji, jina la mtu mwingine au taasisi au kitu kischoweza kupatikana kwa matumizi kisheria, jina la nembo ya biashara ambayo ina haki miliki ya mtu au taasisi nyingine mbali ya wewe, bila idhini inayostahili. Hautoweza kutumia kama jina la mtumiaji jina lolote lenye kuchukiza, lugha chafu, au matusi.

Vidakuzi

Tunatumia vidakuzi. Kwa kutumia tovuti ya Bizfundi unaridhia kutumia vidakuzi kwa kufungamana na sera ya usiri ya Bizfundi. Tovuti nyingi za kimawasiliano za siku hizi zinatumia vidakuzi ili kutusaidia kupata maelezo ya mtumiaji kila

anapotembelea Tovuti. Vidakuzi vinatumika kwenye baadhi ya maeneo ya tovuti yetu ili kutusaidia utendaji wa eneo husika na kuwarahisishia matumizi wale wanaotembelea tovuti. Baadhi ya taasisi shiriki/washirika wetu wa matangazo ya biashara wanaweza pia kutumia vidakuzi.

Haki Miliki za Kazi za Sanaa

BizFund ina nia ya dhati ya kuheshimu, kuzingaria na kudumisha Haki Miliki za Kazi za Sanaa zote na kuhamasisha watumiaji wake kuziheshimu pia.

.

Haki Miliki za Kazi za Sanaa zote ziwe zimeandikishwa au la, kwenye Tovuti, taarifa ya kimaudhui kwenye Tovuti na usanifu wote wa tovuti, ikiwemo ila haishii tu kwenye, maandishi, michoro, programu za kompyuta, picha, video, miziki, milio, na uchaguzi na mpangilio wake na ukusanyaji programu za kompyuta, na chanzo cha msimbo husika na programu za kompyuta vitabaki kuwa mali yetu. Maudhui yote ya Tovuti pia vinalindwa na haki miliki kama kazi za pamoja chini ya sheria za haki miliki za Tanzania, Marekani, na mikataba ya kimataifa iliyoridhiwa. Haki zote zimehifadhiwa,

Nembo zetu za biashara na vazi la kibiashara havitoweza kutumika kwenye bidhaa au huduma yoyote kabla ya kwanza kupata ridhaa ya kimaandishi ya International Executive Service Corps. Haki Miliki za Kazi za Sanaa zote zimehifadhiwa. Unaweza kutazama na/au kuchapisha kurasa kutoka kwenye http://www.bizfundi.or.tz kwa matumizi yako binafsi kulingana na mipaka iliyowekwa kwenye Kanuni na Masharti. Haupaswi

- Kurudia kuchapisha makala kutoka http://www.bizfundi.or.tz
- Kuuza, kukodisha au kutoa leseni ndogo ya makala kutoka http://www.bizfundi.or.tz
- Kurudia kuzalisha, kudurufua au kutoa nakala ya makala kutoka http://www.bizfundi.or.tz
- Kurudia kusambaza maudhui kutoka http://www.bizfundi.or.tz (isipokuwa tu pale maudhui yametengenezwa mahsusi kwa ajili ya kurudiwa kusambazwa)
-
-

Utoaji taarifa kuhusu uwezekano wa ukiukaji wa Haki Miliki Kazi za Sanaa

Inapotokea kuamini kuwa makala au maudhui yaliyochapishwa kwenye Tovuti yanawaeza kukiuka haki miliki yako au ya mtu mwingine, tafadhali wasiliana nasi. Katika hali hii:

- Madai ya ukiukaji wa Haki Miliki za Kazi za Sanaa yanayofanywa na mtumiaji yuleyule ndani siku tano baada ya kutoa lalamiko la kwanza yatahesabiwa kama lalamiko moja. Lalamiko la kwanza litafikiriwa.
- Mwenye Haki Miliki za Kazi za Sanaa lazima atoe ushahidi wa Haki Miliki za Kazi za Sanaa iliyokiukwa pale anapotoa lalamiko dhidi ya mtumiaji mwingine.
- Plae mtumiaji atapokuwa amepokea onyo au maonyo dhidi ya ukiukaji. BizFundi ina haki ya kukataa au kuzuia ushiriki wa mtumiaji kwenye tovuti na vituo shiriki vya BizFundi.
- Inapotokea kuwa na ukaidi uliokithiri wa kutotii, BizFundi ina haki ya kuzima mara moja akaunti ya mtumiaji bila taarifa yoyoyte.
- Maonyo yanahesabiwa kwa pamoja kila baada ya miezi sita, hii ina maananisha kuwa kila ukiukaji wowote unabaki kwenye kumbukumbu kwa siku 182 baada ya ukiukaji wa kwanza, isipokuwa tu pale akaunti ya mtumiaji itapokuwa imezimwa.

Watumiaji ambao akaunti zao zitakuwa zimezimwa kwa ajili ya ukiukaji wa Haki Miliki Kazi za Sanaa i wanapigwa marufuku kwenye tovuti na wanaweza wakakabiliwa na mashataka na au hatua zaidi za kisheria, pale watakapojaribu kufungua akaunti mpya kwa kutumia jina jingine.

Maoni ya Mtumiaji

Makubaliano haya yanapaswa kuanza tarehe tajwa ya hapa.

Baadhi ya shemu ya tovuti hii zinatoa fursa kwa watumiaji kutuma na kubadilishana maoni, taarifa, makala na taarifa (‘Maoni’) kuhusu maeneo ya tovuti. BiziFundi haichuji, kuhariri, kuchapisha au kupitia maoni kabla ya kuonekana kwenye Tovuti.; Hivyo, maoni hayawakilishi mitazamo au maoni ya BizFundi, mawakala wake, au taasisi zake shiriki. Maoni yanawakilisha mitazamo au maoni ya mtu anayetuma mitazamo au maoni hayo. Kwa kadri inavyoruhusiwa na sheria zilizopo, BizFundi haitahusika au kuwajibika kwa Maoni au hasara, dhima, uharibifu au gharama zitakazosababishwa au zitakazo kuwa na athari itokanayo na matumizi yoyote na/utumaji wa na au uonekanaji wa Maoni kwenye Tovuti hii.

BizFundi itabaki na haki ya kufuatilia Maoni yote na kuondoa Maoni yoyote ambayo kwa utashi wake pekee itayaona kuwa hayako sawa, ya kuchukiza au vinginevyo yanakiuka Kanuni na Masharti haya.

Unatuthibitishia na kuhakikisha kuwa:

- Una stahiki ya kutuma Maoni kwenye Tovuti yetu na una leseni zote muhimu na unaridhia kufanya hivyo;
- Maoni yako hayakiuki Haki Miliki Kazi za Sanaa yoyote, ikiwemo ila haishii kwenye kudurufua, haki miliki za kazi za ugunduzi au nembo ya biashara, au haki miliki ya mtumiaji mwingine yeyote;
- Maoni hayana makala yoyote, ya kuchafua, kukashifu, kuchukiza, yasiyo ya kistaarabu au vinginevyo makala inayovunja sheria au yale yanayoingilia faragha;
- Maoni hayatotumika kuomba au kukuza biashara au desturi au kuwasilisha shughuli za kibiashara au shughuli iliyo kinyume cha sheria.

Kwa hiyo hapa unairuhusu BizFundi leseni isiyo na mipaka ya mrahaba ya kutumia, kuzalisha, kuhariri na kuidhinisha wengine kutumia, kuzalisha, kuhariri maoni yako yoyote katika mfumo au mifumo yote, miundo au chombo cha habari

Anwani Za Mitandano Kwenye Tovuti Zingine

Huduma yetu inaweza kuwa na anwani za mtandao za tovuti za washiriki wengine au huduma ambazo hazimilikiwi au kudhibitiwa na International Executive Service Corps.

International Executive Service Corps haina mamlaka juu ya, na haibebi jukumu lolote kuhusu maudhui, sera za kutunza faragha, au mienendo ya tovuti au huduma ya mshiriki mwingine yeyote.Hatuthibitishi kufanya utoaji wowote wa vyombo/watu hawa au tovuti zao.

Unakiri na kukubali kuwa International Executive Service Corps haitahusika wala kuwa na dhima ya moja kwa moja au vinginevyoa, kwa uharibifu au hasara iliyosababishwa au kudaiwa kusababishwa na au kuhusiana na matumizi au utegemeaji wa maudhui kama hayo, bidhaa au huduma zipatikanazo kwenye au kupitia tovuti au huduma zozote za mshiriki mwingine.

Tunakushauri sana kusoma kanuni na masharti na sera za faragha za tovuti au huduma yoyote ya mshiriki mwingine unayoitembelea.

Kuunganishwa kwenye Maudhui yetu

Asasi zifuatazo zinaweza kujiunga kwenye Tovuti yetu bila ya kuwa na taarifa ya kimaandishi kwanza.

- Programu za kutafutia vitu mtandaoni;
- Asasi za habari;
- Wasambazajai wa saraka mtandaoni wanapotuorodhesha kwenye saraka wanaweza kujiunga kwenye Tovuti yetu kwa namna ileile wanayoitumia kujiunga kwenye Tovuti zingine za biashara zilizoorodheshwa; na Biashara Zilizothibitishwa Kimfumo isipokuwa asasi zisizo za kibiashara, maduka makubwa ya misaada, na makundi ya kuchangisha fedha za misaada ambayo yanaweza kutojiunga kwenye Tovuti yetu.

Asasi hizi zinaweza kujiunga kwenye ukurasa wetu, kwenye machapisho yetu au kwenye taarifa za Tovuti zingine ili mradi tu anwani ya kujiunga: (a) haipotoshi kwa namna yoyote; (b) haina udanganyifu wa kumaananisha kuwa ni ufadhili, kuthibitisha au kuidhinisha kwa upande ule unajiunga na bidhaa au huduma zake; na (c) inaingia vyema katika muktadha wa tovuti ya upande inazojiunga nao.

kwa maamuzi yetu pekee tunaweza kufikira na kuidhinisha maombi mengine ya kujiunga kutoka kwenye aina ya asasi zifuatazo: Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA); Msajiri wa Asasi za Kiraia , ijulikanayo kama tovuti za kijamii za dot.com za vyanzo vya taarifa za mlaji na / au biashara; vyama au vikundi vingine vinavyowakilisha mashirika ya misaada, ikiwemo tovuti za utoaji misaada, wasambazi wa saraka mtandaoni, milango ya taarifa za mtandao (Portals), makampuni ya kihasibu, sheria na ushauri ambao wateja wake wakubwa ni wafanyibishara, taasisi za kielimu na vyama vya kibiashara.

Tutaidhinisha maombi ya kujiunga kwenye anwani za mtandao kutoka kwenye asasi hizi pale tutapojihakikishia kuwa; (a) anwani haitatuakisi vibaya sisi au shughuli zetu zilizothibitishwa (kwa mfano vyama vya kibisahara au asasi nyingine ambazo kimsingi zinawakilisha aina za biashara zenye kutia shaka, mfano fursa za kufanya kazi ukiwa nyumbani, hizi hazitaruhusiwa kuunganishwa); (b) asasi ambazo hatuna kumbukumbu zake za kuridhisha, (c) faida kwa upande wetu inayotokana na kufahamika kwetu kunakotokana na kujiunga huku kunazidi kutokuwapo kwake, na (d) pale anwani inapokuwa kwenye muktadha wa maelezo ya jumla au vinginevyo inaenda sambamba na maudhui ya kiuhariri wa kwenye kijarida au bidhaa kama hiyo inayo endeleza dhamira ya asasi.

Asasi hizi zinaweza kujiunga kwenye ukurasa wetu, kwenye machapisho yetu na kwenye maelezo ya Tovuti zingine ili mradi tu anwani ya kujiunga: (a) haipotoshi kwa namna yoyote; (b) haina udanganyifu wa kumaananisha kuwa ni ufadhili, kuthibitisha au kuidhinisha kwa upande ule unajiunga na bidhaa au huduma zake; na (c) inaingia vyema katika muktadha wa tovuti ya upande inazojiunga nazo.

Kama ni miongoni mwa asasi zilizoorodheshwa kwenye ibara ya 2, na una hamasa ya kujiunga na Tovuti yetu, unapaswa kutuarifu kwa kutuma barua pepe kwenda bizfundi@iesc.org.

Tafadhali weka jina lako, jina la asasi yako, taarifa za mawasiliano (kama vile namba ya simu na/au anwani ya barua pepe) pamoja na anwani ya mtandao ya tovuti yako, orodho za anwani za mtandao unazokusudi kuziunga kwenye Tovuti yetu, na orodha ya anwani za mtandao kwenye Tovuti yetu unazopenda kujiunga nazo. Tupe wiki 2 hadi 3 kabla ya kukupa jibu.

Asasi zilizothibitishwa zinaweza kujiunga kwenye Tovuti yetu kama ifuatavyo:

- Kwa kutumia jina letu la Kampuni; au
- Kwa kutumia anwani ya Tovuti (Anwani ya Mtandao) inayounganishwa kwake; au
- Kwa kutumia aina nyingine yoyote ya maelezo ya Tovuti yetu au makala inayounganishwa kwake na yenye mantiki katika muktadha na mfumo wa maudhui ya tovuti ya upande inakounganishwa kwayo.

Matumizi yoyote ya nembo au kazi za Sanaa za Bizfundi hayataruhusiwa katika kuunganisha makubaliano ya leseni ya nembo ya biashara ambayo hayapo.

Fremu

Bila kuwa na idhini ya na ruhusa dhahiri ya kimaandishi, hautoweza kutengeneza fremu kuzunguka kurasa za Tovuti zetu au kutumia mbinu nyingine zitakayobadilisha kwa namna yoyote muonekano au taswira ya Tovuti yetu.

Uondoaji wa anwani ya mtandano kwenye tovuti yetu

Utakapoona anwani yoyote kwenye Tovuti yetu au tovuti yoyoyte iliyounganishwa kwayo kuwa haikubaliki kwa sababu yoyote, unaweza kuwasiliana na sisi kuhusu kadhia hiyo. Tunaweza kufikiria maombi ya kuziondoa anwani hizo bali hatutakuwa na wajibu wa kufanya hivyo au kurudisha majibu moja kwa moja kwako.

Wakati tukijitahidi kuhakikisha kuwa taarifa kwenye tovuti hii ni sahihi, hatuwezi kuahidi utimilifu au usahihi wake, hatuwezi pia kujipa jukumu la kuhakikisha kuwa tovuti inaendelea kupatikana au makala za kwenye tovuti zinakuwa ni za hivi karibuni wakati wote

Usitishwaji

Pamoja na marekebisho yoyote ya kisheria au yanayolingana na hayo, tunaweza bila kukupa taarifa, kusitisha mara moja Kanuni na Mashrati au kubatilisha haki yako

yoyote au haki zote ulizopewa chini ya Kanuni na masharti haya. Baada ya mkataba huu kusitishwa, utakoma mara moja kupata au kutumia Tovuti, na pamoja na marekebisho yoyote ya kisheria au yanayolingana na hayo, tutabatilisha nenosiri au manenosiri yote na utambulisho wa akaunti uliokuwa umepewa na utazuiliwa kupata au kutumia sehemu moja ya au Tovuti nzima. Usitishwaji wowote wa makubaliano haya hauta athiri haki zingine na majukumu ya mshirika (ikiwemo na bila kuishia kwenye, majukumu ya malipo) yaliyokuwapo kabla ya tarehe ya usitishwaji. Vilevile unaafiki kuwa Tovuti haitakuwa na dhima kwako au kwa mtu yeyote inatakayotokana na usimamishwaji au usitishwaji. Kama hauridhiki na Tovuti au na, kanuni, masharti, sheria, sera, miongozo au mienendo yoyote ya uendeshaji wa Tovuti, ufumbuzi ulinao pekee ni kuacha kutumia Tovuti.

Mashart yote ya Kanuni ambazo kwa asili yake yanapashwa kuendelea hata baada ya usitishwaji yataendelea baada ya usitishwaji, ikiwemo ila bila kuishia kwenye, masharti ya umiliki, ruhusa ya makanusho,, fidia na mipaka ya dhima.

Ulipaji Fidia

Unakubali kulinda, kufidia na kutoidhuru International Executive Service Corps, na wenye leseni na watoa leseni, na waajiri wao, makandarasi, mawakala, maafisa na wakurugenzi, kutokana na na dhidi ya dai au madai yoyote, uharibifu, majukumu, hasara, dhima, gharama au madeni na matumizi (ikiwemo ila bila kuishia kwenye ada za wakili), yatokanayo na au yaliyojitokeza kufuatia a) matumizi na upataji wako wa Huduma, yaliyofanywa na wewe au mtu mwingine kwa kutumia akaunti au neno siri lako; b) ukiukaji wa Kanunii, au c) Maudhui.

Watumiaji wanakubali kuwa BizFundi haitafungwa na dhima yoyote kwenye mkataba, kabla ya mkataba au uwakilishi mwingine , kwenye ukiukaji wa haki ya mtu, ikiwemo ila bila kuishia kwenye, uzembe, au vinginevyo kutokana na au kuhusiana na Kanuni na Masharti kwa hasara zozote za kiuchumi, kama vile, ila bila kuishia kwenye faida, akiba zilizotarajiwa, mapato, mikataba au biashara kiujumla, upotezaji imani au sifa; na hasara zozote maalum au zisizo za moja kwa moja zilizomuathiri au kumtokea mmoja wa washirika zilizotokana na au zinazohusiana na masharti ya jambo lolote chini ya Kanuni na Masharti haya. Watumiaji wanakubali kuwa BizFundi haitawajibika au kuwa na dhima kwa upotevu wa maudhui au makala iliyowekwa au kutumwa kupitia tovuti na haikubali dhima ya aina yoyote kwa upotevu au uharibifu kwa hatua iliyochukuliwa au itakayochukuliwa kuhusiana na kitu au maelezo yaliyo kwenye tovuti. Watumiaji wanakubali kuwa BizFundi haithibitishi kuwa huduma zetu zitapatikana wakati wote, bila kukatikakatika au kuwa huduma hizo zitakuwa salama; hivyo uendeshaji wa tovuti unaweza kukatishwa kwa sababu nyingi mbalimbali na zilizo nje ya uwezo wetu. Kwa kuongezea, Tovuti na Huduma vinatolewa ‘kama zilivyo, pale zilipo’, na

pale na wakati zinapopatikana, na kwa kadri inavyoruhusiwa na sheria za nchi, ruhusa zote zinazomaananishwa, masharti au Kanuni zingine, iwe zmemaananishwa kwenye sheria au vinginevyo, ikiwmo ila haiishii, kwenye kanuni zozote kuhusiana na stadi na utunzaji au utendaji kwa wakati vimeachwa,

Mipaka ya dhima

Haitatokea kwa International Executive Service Corps ama wakurugenzi wake, waajiriwa, washirika, mawakala, wasambazaji, au tasisi shiriki, kuwa na dhima isiyo ya moja kwa moja, dhahiri, maalum, inayotokana na au uharibifu, ikiwemo bila kuishia tu kwenye, upotevu wa faida, taarifa, matumizi, imani, au hasara nyingine zisizoshikika, zitokanayo na i) upataji wako wa au matumizi ya au kushindwa kupata au kutumia Huduma, ii) mienendo au maudhui yoyote ya mtumiaji mwingine yeyote kwenye Huduma, iii) maudhui yoyote yapatikanayo kwenye Huduma, na iv) upatikanaji , matumizi, au ubadilishaji wa chochote unachotuma au maudhui usioidhinishwa, iwe imetokana na ruhusu , mkataba, ukiukaji wa haki ya mwingine, (ikiwemo uzembe) au nadharia yoyote ya kisheria, iwe tumepewa taairafa au la ya uwezekano wa kutokea uharibifu huo; na hata pale rekebisho lililofanyika limeonekana kushindwa kufikia lengo lake la msingi. Kwa kukubaliana na Kanuni na Mashrati haya, umekubali kufidia na kutuacha sisi (na maafisa, wakurugenzi, mawakala, matawi, wabia na waajiri wetu) bila madhara na bila dhima ya lalamiko au dai lolote, ikiwemo ada za wakili, lililofanywa na mshiriki mwingine yeyote kutokana na au iliyojitokeza kufuatia uvunjai wa Makubaliano haya, au ukiukaji wowote wa sheria au wa haki za mshiriki mwingnie.ulioufanya.

.

Utatuaji migogoro

Kunapotokea na mgogoro/kutokuelewana kati yako na yetu, shabaha yetu itakuwa ni kukupatia nyenzo isiyo na gharama na isiyoegemea upande wowote ya kutatua mgogoro kwa haraka. Kwa hali hiyo basi, wewe na sisi tunakubali kuwa tutatatua lalamiko au mzozo wowote wa sheria au wa usawa unaotokana na Makubaliano haya au huduma zetu kufuatana na moja ya vifungu vidogo hapo chini au vinginevyo kadri sisi na wewe tutakavyokubaliana kwa pamoja na kimaandishi. Kabla ya kuamua kuchukua hatua hizi, tunakuhimiza sana kwanza kuwasiliana na sisi moja kwa moja ili kupata ufumbuzi. Tutayafikiria maombi yale tu yenye busara ndani yake katika kutatua miogogoro kupitia taratibu mbadala za kutatua migogoro, kama vile usuluhishi, na madai ikiwa ni hatua ya mwisho.

Mzozo, dai, au mgogoro unatokana na au unaohusiana na Kanuni na Masharti haya yatapelekwa kwa na kisha kutatuliwa kupitia usuluhishi wa faragha na wa siri unao

mfunga kila mshiriki mbele ya msuluhishi mmoja aliopo nchini Tanzania kwa Kiingereza kwa kufuata sheria za Tanzania na kwa kuzingatia Sheria ya Usuluhishi Kifungu cha 15 ya mwaka 2002 ya Tanzania, kama inavyofanyiwa marekebisho, kubadilishwa na kutungwa tena mara kwa mara. Msuluhishi atakuwa ni mtu ailiyepata mafunzo ya sheria na mwenye uzoefu kwenye fani ya tekinolojia ya habari Tanzania na asiyeegemea upande wowote. Mbali na pamoja na maelezo yaliyotangulia, Tovuti inabaki na haki za kutafuta msaada wa utunzaji wa Haki Miliki ya kazi za Sanaa na usiri wa taarifa kupitia amri za kisheria au hatua nyingine stahiki kupitia mahakama.

Ufaragha wa Taarifa, Ulinzi na Usalama

Hatutakuuzia or kuwapatia maelezo yako binafsi washiriki wengine kwa malengo yao ya kibiashara kabla ya kwanza kupata ridhaa yako. Tutatumia taarifa yako kwa namna tu ilivyoelezewa kwenye Sera yetu ya Ufaragha na Usiri. Tunachukulia utunzaji wa siri ya mtumiaji kama jukumu muhimu sana la kijamii. Tunahifadhi na kuchakatua taairafa yako kwenye kompyuta zinazolindwa kwa vifaa vya ulinzi yenye umadhubuti wa kifizikia na kitekinolojia. Unaweza kupata na kuboresha taarifa unayotupatia na kuamua kutopokea baadhi ya mawasiliano kwa kuingia kwenye akaunti yako. Tunatumia washiriki wengine kuhakiki na kuthibitisha kanuni zetu za usiri. Kama hupendi taarifa yako kutumwa au kutumika kwa namna hii tafadhali usitumie huduma zetu.

Hakuna uwakala

Hakuna mahusianao ya uwakala, ushirikiano, ubia, mwajiri-mwajiriwa au mwakilishwa-mwakilishi yanayokusudiwa au kutengenezwa na Makubaliano haya.

Vivuo

Baadhi ya mamlaka haziruhusu kuondolewa kwa ruhusa fulani au kuondolewa kwa mipaka ya dhima kwa uharibifu wa kusababishwa au wa kidharura, hivyo mipaka ya hapo juu inaweza isikuhusu wewe.

Iwapo sehemu yoyote ya Kanuni na Maharti haya yatachukuliwa na mahakama kuwa nia batili au kutotekelezeka, aidha sehemu yake au yote kwa ujumla wake, basi sehemu hiyo itaondolewa kwenye Kanuni na Mashrati haya na hayata athiri uhalali au utekelezekaji wa sehemu myingine yoyote iliyoorodheshwa kwenye nyaraka huu.

Sheria Itakayosimamia

Kanuni na Mashrti haya yatatafsiriwa na kusimamiwa na sheria zinazotumika kwenye Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Pamoja na kuzingatia Kipengele cha Utatuaji Migogoro hapo juu, kila upande unakubali kuheshimu mamlaka za Mahakama za Tanzania na kuondoa mapingamizi yoyote kuhusiana na mahali.

Kushindwa kwetu kutekeleza haki au sharti lolote kwenye Kanuni hizi hakutachukuiliwa kuwa ni kuondolewa kwa haki hizo. Kama kila sharti la Kanuni hizi itachukuliwa na Mahakama kuwa ni batili au haitekelezeki, masharti yanayobakia ya Kanuni hizi yataendelea kutumika. Kanuni hizi zinajumuisha makubaliano yote baina yetu kuhusiana na Huduma zetu, na yako juu na yanabatilisha makubaliano yoyote ya awali ambayo tungeweza kuwa nayo baina yetu kuhusiana na Huduma.

Taarifa na Marekebisho

Tunabaki na haki, kwa matakwa yetu pekee, ya kuboresha au kubadilisha Kanuni hizi wakati wowote. Kama marekebisho ni makubwa tutatoa walau siku 30 kabla ya kanuni zozote mpya kuanza kutumika. Kinachofanya marekebisho kuwa makubwa kitaamuliwa na sisi na kubaki ndani ya maamuzi yetu pekee.

Tutatuma taarifa kwako kupitia barua pepe kwa kutumia anwani ya barua pepe uliyoitoa BiFundi wakati wa mchakato wa kujiandikisha. Taarifa itachukuliwa kuwa imetumwa na kupokelewa masaa 24 baada ya barua pepe kutumwa, labda pale mtumaji anapoarifiwa kuwa anwani ya baura pepe ni batili. Vinginevyo, tunaweza kukupa taarifa ya kisheria kwa njia ya barua ya rejista kwenye anwani iliyotolewa wakati wa mchakato wa kujiandikisha. Taarifa zinazotumwa kwako kupitia barua ya rejista zitachukuliwa kuwa zimepokelewa na upande husika siku tatu baada ya tarehe ya kutumwa. Kwa kuendelea kupata au kutumia Huduma zetu baada ya marekebisho kuanza kutumika, unakubali kujifunga kwenye kanuni zilizofanyiwa marekebisho. Kama haukubaliani na Kanuni mpya basi hauruhusiwi kutumia Huduma

Masharti Mtambuka

Unakubali kuwa makubaliano yote, taarifa, maungamo na mawasiliano mengine tunayokupatia kielektroniki yanakidhi matakwa yote ya kisheria yanayotaka mawasiliano kama hayo yawe ya kimaandishi. Hairuhusiwi kutoa au kuingia mkataba mdogo wa haki zozote au majukumu yako chini ya Kanuni na Masharti haya kwa mshiriki mwingine yeyote, isipokuwa tu pale panapokuwa na makubaliano ya kimaandishi na muuzaji. Tunabaki na haki ya kuhamisha, kutoa au kugawa manufaa ya sehemu au ya haki au majukumu yote kwa mshiriki mwingine yeyote chini ya Kanuni na Masharti haya

Wasiliana nasi

Kama una maswali yoyote kuhusu Kanuni hizi, tafadhali wasiliana nasi kupitia bizfundi@iesc.org.

Kanusho

UNAELEWA NA KUKUBALI KUWA MAUDHUI YOYOTE YANAYOPAKULIWA AU VINGINEVYO KUPATIKANA KUPITIA MATUMIZI YA TOVUTI NI KWA MAAMUZI YAKO NA USALAMA WAKE NI JUKUMU LAKO, NA KWAMBA WEWE MWENYEWE NDIYE UTAKAYEHUSIKA NA UHARIBIFU WOWOTE KWENYE MFUMO WAKO WA KOMPYUTA AU UPOTEVU WA TAARIFA AU KATISHO LA KAZI LITOKANALO NA UPAKUAJI WA MAUDHUI. HATUTAHUSIKA NA UPOTEVU AU UHARIBIFU WOWOTE, UTAKAOSABABISHWA, AU UTAKODAIWA KUSABABISHWA, MOJA KWA MOJA AU VINGINEVYO, NA TAARIFA AU MAWAZO YALIYOMO, YAPENDEKEZWAYO AU KUREJEREWA KWENYE AU YAONEKANAYO KWENYE TOVUTI. USALAMA WA USHIRIKI WAKO KWENYE TOVUTI NI JUKUMU LAKO WEWE MWENYEWE. HAKUNA USHAURI AU TAARIFA, IWE YA MDOMO AU KIMAANDISHI , UIPATAYO KUTOKA KWETU AU KUPITIA WAAJIRIWA WETU, AU WASHIRIKI WENGINE ITAKAYOTENGENEZA RUHUSA AMBAYO HAIJAELELEZWA HUMU KIFASAHA..

DHIMA YETU YA JUMLA KWA DAI LOLOTE AU MADAI YOTE KUHUSIANA NA TOVUTI HAITAZIDI FEDHA ZA KITANZANIA ELFU KUMI (10,000/=). MTUMIAJI ANAKUBALI NA KUKIRI KUWA MIPAKA ILIYOWEKWA KUHUSU DHIMA NI MSINGI MUHIMU WA MAPATANO YA BEI NA HATUTAWEZA KUWA NA TOVUTI ISIYO NA MIPAKA HII.